SIGNAL Publishers

Igniting thinking

GREDI YA 9 - 2025

# SIGNAL CBC ASSESSMENT
# JARIBIO LA NNE

THE SCHOLAR
004

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

**— KISWAHILI KARATASI YA 1—**

**MUDA: SAA 1 DAK 30**

JINA: ..................................................

GREDI: ..................................................

SHULE: ..................................................

NAMBARI YA TATHMINI: ..................................................

**Maagizo kwa mwanafunzi:**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Soma kila swali kwa makini
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.
5. Nakili sahihi yako katika kiapo kilicho chini ya ukurasa huu.

**JEDWALI LA ALAMA**

| Zoezi | Alama za jumla | Alama za mwanafunzi | Upeo |
|---|---|---|---|
| Sehemu A: Ufahamu | 25 | | |
| Sehemu B: Kihasho | 10 | | |
| Sehemu C: Sarufi | 15 | | |
| | 50 | | |

**Kiapo: "Naapa kutokiuka sheria zozote wakati wa mtihani huu".**

**Sahihi: ....................................................** **Tarehe: ....................................................**

## SEHEMU A: KUSOMA UFAHAMU (alama 25)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 9***

Hapo zamani za kale, katika nchi ya Nuru, paliishi kijana aliyeitwa Mwamba. Kijana huyo alienziwa sana na wakazi wengine kutokana na nguvu na jitihada zake za kuitetea jamii yake. Wakazi wengi walitegemea kilimo cha mimea na ufugaji wa wanyama. Mara kwa mara, mahasidi zao waliwavamia kwa azma ya kuiba mifugo lakini kila walipofika, Mwamba aliwaongoza mashujaa wenzake wakawasukuma maadui wale hadi nje ya mipaka yao. Wale waliodiriki kuonyesha ukaidi waliangushwa na upanga wa Mwamba.

Miaka ilizidi kusonga hata ukafika wakati wa Mwamba kupata jiko. Alitafutiwa mabinti wote warembo kutoka jamii yake lakini akakataa katakata kuwaoa. Alisema kwamba anataka mke katika nchi ya mbali. Wazee wake walimpa radhi zao akafunga safari asubuhi moja.

Baada ya kupiga milundi kwa juma zima, Mwamba alijipata katika nchi ya Mavuno. Wenyeji wa huko walikuwa waja wakarimu na wenye mioyo safi. Mwamba alipokelewa kwa mikono miwili na kila familia aliyoitembelea. Mabinti wa huko walikuwa hurulaini. Haukupita muda, Mwamba akampata mmoja aliyempendeza akaamua kumwoa.

Utamaduni wa Mavuno ulimhitaji mtu amsaidie baba mkwe katika kazi zake kwa mwezi mmoja kabla ya kukabidhiwa mke. Baada ya hapo, mtu na mchumba wake wangepelekwa mbele ya baraza la wazee wafanyiwe tambiko ili kuwakinga dhidi ya mikosi ya aina yoyote. Mwamba alipoarifiwa hayo, alicheka hadi mbavu zikavunjika. Alidai kwamba yeye alikuwa radhi kulipa kiasi chochote cha mahari almradi asishiriki utamaduni wowote wa kishenzi. Juhudi za kumrai asipuuze kaida hizo ziliambulia patupu. Mwishowe wazee wakaamua kuwa, mtoto akililia wembe mpe.

Mwamba alimchukua mchumba wake bila baraza za wazee akashika tariki kurudi nyumbani. Moyoni aliona fahari kwa ushindi wake. Njiani alikuwa akiimba nyimbo ambazo kwa kawaida waliimba na wenzake kila walipopata ushindi dhidi ya mahasimu.



CamScanner

Ghafla bin vuu, walizuka mashujaa waliojihami wakamkabili Mwamba ana kwa ana. Mwamba ni nani? Alipambana nao kiume. Aliwaangamiza wavamizi wale takriban wote. Hata hivyo, alikuwa ameumia vibaya. Wale waliosalia walimchukua mchumba wake wakatoroka. Mwamba alibaki akiuguza majeraha ya mwili na roho.

Laiti Mwamba angalisikiza rai ya wazee hayo yasingalimfika. Mbali na kupokea baraka za wazee, angepewa vijana wa kumsindikiza hadi kwao. Aliwaza hayo yote moyoni lakini akajua kuwa maji yakimwagika hayazoleki.

1. Kulingana na aya ya kwanza
   A. Mwamba alikuwa mkulima hodari
   B. ulikuwepo mgogoro baina ya jamii ya Mwamba na majirani
   C. jamii ya Mwamba ilipenda kushambulia majirani zao
   D. wakazi walistawi kwa uongozi wa Mwamba.
2. Si kweli kusema kuwa
   A. tabia za Mwamba zilibadilika alipokaribia kuoa
   B. wazee walikuwa na nia nzuri kwa Mwamba
   C. jamii ya Mwamba ilikuwa na mabinti wazuri
   D. Mwamba alitaka kutafuta mke mbali na kwao.
3. Wakazi wa nchi ya Mavuno
   A. walikuwa wanafiki
   B. hawakuwa wapiganaji wazuri
   C. hawakupenda kusaidia
   D. waliwapenda wageni.
4. Maneno '**<u>alicheka hadi mbovu zikavunjika</u>**' yametumia mbinu gani ya lugha?
   A. Kinaya  B. Uhuishaji
   C. Chuku  D. Majozi
5. Kwa nini wazee wa Mavuno hawakumbariki Mwamba?
   A. Alipuuza utamaduni wao.
   B. Alizua vita ugenini.
   C. Hawakuridhishwa na mahari aliyotoa.
   D. Alikuwa mgeni katika jamii yao.
6. Ni sifa ipi haiambatani na mienendo ya Mwamba kati ya hizi?
   A. Mzalendo  B. Shujaa
   C. Mtiifu  D. Mkaidi
7. Mwamba alipokuwa akirudi nyumbani
   A. alishambuliwa na vijana kutoka Mavuno
   B. alivamiwa akampoteza mchumba wake
   C. aliwashinda maadui akaimba nyimbo za ushindi
   D. alisindikizwa na wenyeji waliomsaidia kupigana.
8. Chagua methali ifaayo zaidi kujumuisha ujumbe wa hadithi hii.
   A. Kwa mwoga huenda kicheko kwa shujaa huenda kilio.
   B. Baada ya dhiki ni faraja.
   C. Mwenye nguvu mpishe.
   D. Majuto ni mjukuu huja baadaye.
9. Neno **azma** limetumika katika kifungu hiki. Chagua neno jingine lenye maana sawa na hilo.
   A. Sababu  B. Kusudi
   C. Uvamizi  D. Hatima

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 10 hadi la 18.</u>***

Maliasili ni vitu vyote vinavyotokana na maumbile kama vile madini, misitu, wanyamapori, bahari, mito na maziwa ambayo hupatikana katika mazingira yetu. Japo binadamu mwenyewe hakuhusika katika kuumba maliasili, hana budi kuzitunza na hata kuongeza thamani pale awezapo. Hata hivyo, inasikitisha kumwona binadamu yuyo huyo, kwa kuongozwa na tamaa iliyokithiri, akiziharibu maliasili kiholela.

Misitu ni maliasili muhimu. Ni ukweli usiopingika kuwa misitu ndiyo huchangia katika kuvuta mvua. Mahali palipo na misitu hupata mvua inayotegemewa msimu baada ya msimu. Ni muhali kwa wakazi wa mahali kama hapo kushindwa kujitosheleza kwa chakula. Mbali na hayo, misitu ni makazi ya wanyama na ndege mbalimbali. Kuna watu ambao huikata mti katika misitu kiholela kwa tamaa ya kutajirika upesi kwa kuuza mbao au kuchoma makaa. Huko ni **<u>kujipalia makaa</u>**. Tunapaswa kuitunza misitu ili tusikaushe vyanzo vya maji. Aidha, tuendelee kupanda miti ya kiasili na ya kisasa katika misitu ili tujivunie manufaa ambayo ni tumbi nzima.

Mito, maziwa na bahari ni maliasili muhimu sana nchini. Biashara ya uvuvi huendeshewa humo. Bila shaka, ni vitegauchumi muhimu kwa wavuvi wengi. Isitoshe, maji yanayopatikana humo hutumiwa katika shughuli za nyumbani, zaraa na hata viwandani.

Mara nyingi maji ya mito huchafuliwa kwa kemikali zenye sumu kutoka nyumbani, mashambani, viwandani na kwingineko. Matokeo yake huwa vifo vya wanyama mbalimbali wa majini. Meli zinazosafirisha mafuta, shughuli za kujistarehesha na mabadiliko ya tabia-nchi ni tishio kwa mito, maziwa na bahari zetu. Ni vyema kukomesha vitendo vinavyoharibu maji yetu tusije kuathirika. Tukumbuke kuwa msiba wa kujitakia hauna kilio.

Jukumu la kutunza maliasili ni la kila mwananchi. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Tuungane kupanda miti kwa wingi. Tufanye bega kwa bega shughuli za usafi katika kingo za mito, fuo za bahari na maziwa yetu. Tuwatunze Wanyama wetu na kuwashtaki majangili ili wafunguliwe mashtaka. Kwa vyovyote vile, tusijipakatie mikono na kudai kuwa huo ni wajibu wa serikali.

10. Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu.
    A. Baadhi ya maliasili huundwa na binadamu.
    B. Binadamu hana uwezo wa kuboresha maliasili.
    C. Binadamu ana wajibu wa kutunza na kuboresha maliasili.
    D. Uwepo wa maliasili huleta usumbufu kwa binadamu.

11. Upi si mfano wa maliasili kulingana na kifungu?
A. Mabwawa ya maji B. Wanyamapori
C. Misitu D. Bahari

12. Vitendo vya binadamu katika kifungu vinaonyesha kuwa ni mwenye
A. uwajibikaji B. umoja
C. uangalifu D. tamaa.

13. Kulingana na kifungu, eneo lenye misitu
A. hupata mvua wakati wote
B. huwa na mazingira bora ya kilimo
C. huwa na uhaba wa chakula
D. halina shughuli nyingi za kiuchumi.

14. Yafuatayo ni madhara ya ukataji wa misitu isipokuwa
A. upatikanaji wa kuni na makaa
B. kuangamiza makazi ya ndege na wanyama
C. kukauka kwa vyanzo vya maji
D. kupungua kwa mvua.

15. Iwapo maji ya mito, maziwa na bahari yatachafuliwa
A. shughuli za uchukuzi zitatatizika
B. wanyama watapungua katika misitu
C. shughuli za kujistarehesha zitaathiriwa
D. wavuvi watakosa riziki yao.

16. Mwito wa mwandishi wa makala haya ni kuwa
A. tushirikiane kuvuruga maliasili
B. tuwajibike katika kuhifadhi maliasili
C. tuepuke matumizi ya maji viwandani
D. meli zinazosafirisha mafuta ziondolewe.

17. Kwa jumla, kifungu hiki kinahusu
A. aina za mahasili B. wingi wa maliasili
C. uhifadhi wa maliasili D. maovu ya binadamu.

18. Msemo '<u>kujipalia makaa</u>' umetumiwa katika kifungu hiki. Msemo huo una maana ya
A. kutaabika sana B. kujuta
C. kujivunia D. kujiletea shida.

*<u>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 19 hadi la 25.</u>*

*(Babu ameketi na wajukuu wake chini ya mti)*

**Vijana:** Shikamoo babu?

**Babu:** Marahaba wajukuu wangu. Nimefurahi sana kwa kuwaona.

**Halima:** Nasi tumefurahi pia babu. Siku zote sisi hufurahia kusikiliza ngano zako tamutamu zilizojaa mafunzo.

**Babu:** *(Akizima redio aliyokuwa akisikiliza)* Mwajua nimesikia habari za kuatua moyo kwenye redio. Habari zenyewe zimeniacha na huzuni tele.

**Boru:** Habari zipi babu? Wajua siku hizi dunia imejaa vituko.

**Babu:** Taarifa zenyewe ni kuhusu kijana aliyejaribu kujitia kitanzi.

**Vijana:** *(Wakionyesha mshtuko)* Lo!

**Bela:** Siku hizi vijana wengi wana matatizo ya kikatili. Japo wanaonekana wazima barabarani, wengi wao wana msongo wa mawazo.

**Halima:** Naam, tulijadili hayo darasani. Wapo vijana wanaoathiriwa na mihadarati wengine nao, kwa kuengwaengwa na wazazi na walezi wao wanashindwa kukabiliana na changamoto za maisha.

**Bela:** Babu, nyinyi mlipokuwa vijana hakukuwa na matukio kama haya?

**Babu:** Kama yalikuweko, basi yalikuwa machache sana. Siku hizo, tulijitenga na dawa za kulevya. Pia, tulitafuta ushauri wa wakubwa wetu tulipokabiliwa na changamoto. Siku zote tulikumbuka kuwa jungu kuu halikosi ukoko.

**Boru:** Hata sasa tunaweza kuyaepuka mambo kama hayo. Kupita ushauri wa marika, tunaweza kuelimishana na kutiana moyo bila kupotoshana.

**Babu:** Kesho tutaongea kuhusu njia za kuimarisha afya ya akili. Nitawasimulia kisa cha kuvutia. Kwa sasa naomba tuingie nyumbani tusije tukazizima kwa baridi. *(Halima anambebea babu kibago)*

19. Vijana wale walikuwa wenye nidhamu kwa kuwa
A. walienda alipokuwa babu
B. wanakumbuka yale waliyojifunza
C. walimwamkua babu yao
D. wanajadili masuala mbalimbali.

20. Vifaa vya kidijitali vina manufaa gani kulingana na mazungumzo haya?
A. Kufahamisha matukio mbalimbali yanayojiri.
B. Kuwapotosha vijana.
C. Kuburudisha wanajamii.
D. Kuwatia moyo wanajamii.

21. Habari alizopokea babu zilimwacha katika hali gani?
A. Kuchanganyikiwa B. Masikitiko
C. Uchangamfu D. Kuogopa

22. Kifungu kimeonyesha kuwa wanaokabiliwa na msongo wa mawazo
A. ni rahisi kuwatambua
B. huanza kutumia mihadarati
C. huwa na wasiwasi
D. hawaonyeshi dalili waziwazi.

23. Si kweli kusema kuwa
A. dawa za kulevya husababisha matatizo ya kiakili
B. zamani hakukuwa na visa vyovyote vya matatizo ya kiakili
C. kubembelezwa sana kunaweza kufanya mtoto asiwe mkakamavu maishani
D. shule huwaandaa vijana kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali.

24. Mazungumzo haya yalikuwa na wahusika wangapi?
A. Wanne B. Watatu
C. Kumi na wawili D. Watano



CamScanner

25. Methali '**Jungu kuu halikosi ukoko**' inawahimiza vijana
A. waepuke dawa za kulevya B. wafanye bidii maishani
C. wawe na uvumilivu D. wawaheshimu wazee wao.

**SARUFI**

***Chagua jibu sahihi kujibu swali la 26 hadi 35.***

Watu ......**26**....... na ujuzi wa lugha hutumia tamathali mbalimbali ......**27**...... ujumbe wao .......**28**....... utawasikia wakitumia .......**29**....... kama vile mwafulani ni ndumakuwili, wakiwa na maana kuwa mtu huyo ni .......**30**.......Vilevile, wao hutumia lugha ya adabu.......**31**....... tafsida. Mfano wa tasfida ni .......**32**........

Vipengele .......**33**.......vya lugha ni muhimu sana ....... **34**....... katika kupamba lugha .......**35**....... pia kupunguza ukali wa maneno.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 26. | A. waliyo | B. wako | C. wenye | D. walio |
| 27. | A. kuwasiliana | B. kuwasilisha | C. kuwasilishana | D. kuwasilishwa |
| 28. | A. Mathalani | B. Japo | C. Illali | D. Ingawa |
| 29. | A. tashbihi | B. nahau | C. sitiari | D. tanakali za sauti |
| 30. | A. mnafiki | B. mwoga | C. mjanja | D. mkali |
| 31. | A. uitwao | B. liitwalo | C. kiitwacho | D. iitwayo |
| 32. | A. kuzaa | B. anaendesha | C. ameondoka | D. salaale! |
| 33. | A. hii | B. haya | C. hivi | D. hizi |
| 34. | A. sio tu | B. ndio tu | C. ndivyo tu | D. sivyo tu |
| 35. | A. mbali | B. kama | C. bali | D. sembuse |

***Kuanzia nambari 36 mpaka 50, chagua jibu lifaalo zaidi.***

36. Chagua jawabu lililo na kihusishi cha sababu.
A. Mvua imekuwa ikinyesha tangu asubuhi.
B. Yakobo ameenda hospitalini kwa matibabu.
C. Mtu hafai kuwa mchafu mithili ya fungo.
D. Shamba hilo lililimwa na mkulima yule.

37. Bainisha sentensi inayoonyesha hali ya kufuatana kwa vitendo.
A. Vijana wakielekezwa vizuri watakuwa waadilifu.
B. Wanafunzi walikuwa wakikariri shairi hilo jukwaani.
C. Mazingira yangetunzwa matatizo yangepungua.
D. Mtoto alipelekwa katika kliniki akapewa chanjo.

38. **Kipi ni kielezi katika sentensi ifuatayo?**
Askari wa trafiki walilisimamisha basi hilo barabarani.
A. Wa B. Hilo
C. Barabarani D. Walilisimamisha

39. Chagua sentensi changamano kati ya zifuatazo.
A. Ukuta uliobomoka umejengwa tena.
B. Nyanya anavipalilia viazi vyake.
C. Alishauriwa ili aijiunge na vijana wasiowajibika.
D. Mjomba alikuwa akielekea mjini.

40. **Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.**
"Tutajifunza kuandika insha ya maelezo kesho," mwalimu aliwaambia wanafunzi.
A. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa watajifunza kuandika insha ya maelezo kesho.
B. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa watajifunza kuandika insha ya maelezo kesho.
C. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa wangejifunza kuandika insha ya maelezo siku iliyofuata.
D. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa wangejifunza kuandika insha ya maelezo kesho.

41. **Andika udogo wa sentensi.**
Mtoto huyu atacheza ngoma ile.
A. Toto hili litacheza goma lile.
B. Kitoto hiki kitacheza kigoma kile.
C. Kijitoto hiki kitacheza ngoma ile.
D. Toto hili litacheza ngoma ile.

42. Maagano '**alamsiki**' hujibiwaje?
A. Binuru B. Inshallah
C. Akheri D. Buriani dawa

43. **Andika kauli ya kutendewa ya sentensi:**
Mama anapika uji wa mtoto.
A. Uji wa mtoto unapikwa na mama.
B. Mtoto anapikiwa uji na mama.
C. Mama anampikia mtoto uji.
D. Mama anapikisha uji wa mtoto.

44. **Ingia ni kwa toka kama vilivyo teleka kwa**
A. teua B. vuna
C. telekwa D. epua.

45. Maneno '**ugonjwa**' na '**ubele**' huorodheshwa katika ngeli ipi?
A. U-YA B. U-ZI
C. LI-YA D. U-U

46. **Andika umoja wa sentensi ifuatayo.**
Mikono yao imechafuka.
A. Mikono yake imechafuka.
B. Mkono wao umechafuka.
C. Mkono wake umechafuka.
D. Mkono yake imechafuka.

47. Maji, maziwa na uji ni nomino za
A. wingi B. dhahani
C. makundi D. pekee.

48. **Tegua kitendawili kifuatacho:**
Mfalme wetu hushuka kwa kelele.
A. Usingizi B. Mvua
C. Baridi D. Mwangwi

49. **Kipi ni kitenzi kikuu katika sentensi ifuatayo.**
Kaka alikuwa akiosha vyombo jikoni.
A. Jikoni B. alikuwa
C. akiosha D. vyombo

50. Tambulisha sentensi yenye kiwakilishi cha sifa.
A. Mto huu umechafuliwa lakini ule una maji safi.
B. Mdogo atahudumiwa lakini nyinyi mtasubiri kidogo.
C. Wangu amefika lakini wako atafika baadaye.
D. Mwenyewe amesema kuwa hicho sio chake.



CamScanner